# Karibuni kwa Mwaka wa Shule wa 2025-2026
# Idara ya Huduma za Chakula & Lishe (Food & Nutrition Services)

Spencer Winn, Mkurugenzi wa Huduma za Chakula & Lishe **(314) 345-2320 x72320**
Tenecia Williams, Mtaalamu wa Uwajibikaji **(314) 345-2308 x72308**
Karen Lee, Mtaalamu wa Upishi **(314) 381-4155**

---

Hamjambo Wazazi/ Walezi:

Kwa niaba ya Idara ya Huduma za Chakula na Lishe ya Shule za Umma za Saint Louis niruhuseni kuwakaribisha kirasmi pamoja na wanafunzi wenu kwa mwaka wa shule wa 2025-2026.

SLPS na Chartwell zitaendelea ushirikiano wao mwaka huu wa shule Chartwells ikihudumu kama Kampuni ya Usimamizi wa huduma za Chakula (FSMC). Chartwells itatoa usimamizi wa huduma za usimamizi kwa mikahawa ya shule.

SLPS na Chartwells wanaamini ya kwamba mojawapo ya njia muhimu sana kwa kuweza kuwasaidia wanafunzi Kutenda vema darasani mwao ni kuwapa chakula chenye afya bora na lishe nzuri kila siku shuleni.

**<u>Mpango wa Utoaji kwa Ustahili wa Jamii:</u>**
Shule za Umma za Saint Louis hutenda kupitia Mpango wa Utowaji kwa Ustahili wa Jamii, inayowapa wanafunzi wa shule za SLPS kula bila malipo chakula asubui, mchana, jioni, na vitafunio.

**Idara ya Huduma ya Chakula na Lishe ya SLPS inatekeleza Mipango ifuatayo ya Lishe kwa Watoto inayofadhililiwa na Idara ya Kilimo ya Marakani (USDA), Idara ya Elimu ya Msingi na Sekondari (DESE), na Idara ya Huduma za Afya na Wazee ya Missour**

- Mpango wa Chakula cha Asubui shuleni (SBP)
- Mpango wa Taifa wa Chakula cha Mchana shuleni (NSLP)
- Mpango wa Matunda na Mboga (FFVP)
- Mpango wa Vitafunio Alasiri (ASP)
- Vitafunio Mahiri/Wakusanya Fedha
- Mpango wa Huduma ya Chakula kwa Watoto na Watu Wazima (CACFP)
- Mpango wa Chakula cha Majira ya Joto (SFSP)

**<u>Mpango wa Chakula cha Asubui Shuleni</u>**

- <u>Chakula cha Asubui ni bila kulipa kwa wanafunzi wote. **Watu Wazima Wanalipia Chakula: $2.84.**</u>
- <u>Chakula kinahudumiwa darasani (pk-k) na mikahawa kabla ya shule kuanza</u>
- <u>Chaguo la Chakula moto nafaka, tunda au sharubati ya 100%, maziwa ya kiwango cha chini cha mafuta 1% au maziwa yasiyo na mafuta kabisa.</u>
- **<u>Maziwa yoyote ya ziada yanaweza kununuliwa: meupe- $.60 chokolate: -$.65.</u>**
- <u>Menyu ziko kwenye tovuti ya Shule za Umma za Saint Louis (www.slps.org/menus).</u>

**<u>Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana Shuleni</u>**

***<u>Shule za Msingi</u>*:**

- Chakula cha mchana ni bila malipo kwa wanafunzi wote. **Watu Wazima Wanalipa Chakula: $5.29**.
- Chakula cha mchana ni chaguo la chakula moto chenye afya, nafaka nzima, mboga, chakula cha mboga, na maziwa ya 1% au maziwa ya chokoleti bila mafuta.
- Vyakula vitolewa darasani (pk-k) na mikahawani.
- **Maziwa yoyote ya ziada yanaweza kununuliwa : meupe- $.60 chokoleti- $.65.**
- Menyu ziko kwenye tovuti ya Shule za Umma za Saint Louis (www.slps.org/menus).
- Mwanafunzi atabonyeza enter kwa kifute cha kuuza (POS) chakula cha asubui au mchana.

***<u>Shule za Kati na za Sekondari:</u>***

- Chakula cha mchana ni bila malipo kwa wanafunzi wote. **Watu Wazima Wanalipa Chakula: $5.29**.
- Chakula cha mchana kinajumuisha chakula moto chenye afya, Nafaka nzima, matunda, mboga, chakula cha mboga, na maziwa ya 1% au maziwa ya chokoleti bila mafuta.
- **Maziwa yoyote ya ziada yanaweza kununuliwa: Meupe- $.60 chokoleti- $.65.**
- Matunda na mboga mbichi kwa ajili ya lishe lenye afya.
- Menyu ziko kwenye tovuti ya Shule za Umma za Saint Louis (www.slps.org/menus).
- Kila mwanafunzi atabofya enter kwa kifute cha kuuza (POS) chakula cha asubui au mchana na kuweka Namba ya Utambulisho Binafsi (PIN). PIN ni ile ile kila mwaka.

**<u>Mpango wa Chakula kwa Watoto na Watu Wazima (CACFP): Mpango wa Chakula cha Baada ya Shule</u>**

- Mpango wa Baada ya Shule unaohifadhiwa na Idara ya Huduma za Afya na Wazee.
- Wanafunzi wanapewa lishe tajiri jioni navitafunio.
- Shule zilizo na mpango wa baada ya shule mkiwemo elimu, uboreshaji, na riadha zinastahili kushiriki mpango huu wa baada ya shule.
- Shule zinaweza kupokea chakula cha baridi au cha moto.

**<u>Maelezo ya Ziada kuhusu Lishe</u>**

- Nenda kwa ukurasa wa SLPS: www.slps.org.
  - Kwa kuona muhtasari wa Idara ya Huduma za Chakula na Lishe, nenda kwa www.spls.org bofya kichupo cha **Mzazi & Mwanafunzi,** ndipo **utaona** Muhtasari.
  - Kwa kuona **Sera na Menyu ya Lishe na Barua ya Ukaribisho kwa Wazazi** kwa lugha zao, nenda kwa www.slps.org bofya kichupo cha **Mzazi & Mwanafunzi,** utaona **Sera na Menyu ya Chakula.**
  - Kwa kuona Sera ya Afya na Ustawi, au kuona Sera katika lugha zingine, nenda kwa www.slps.org , bofya **kichupo cha Mzazi & Mwanafunzi**, na nenda kwa **Afya na Ustawi.**
  - Kwa kuona **Namba ya Utambulisho Binafsi (PINs), nenda kwa** www.slps.org , bofya kwa kichupo cha **Mzazi & Mwanafunzi,** nenda kwa **Sera na Menyu ya Chakula.**

Ukiwa na swali lolote, tafadhali wasiliana na Idara ya Huduma za Chakula na Lishe kwa (314) 345-2308.

Tena, ningependa kukushuru kwa msaada na usaidizi wako mwaka huu.

*Spencer Winn*

**Mkurugenzi wa Huduma za Chakula na Lishe**

**Taasisi hii hutoa fursa zilizo sawa.**

# OMBI LA TAARIFA

**(Kila familia itajaza fomu moja)**

Tafadhali jibu swali lililo hapo chini kwa kuweka alama kwa moja ya uru. Taarifa ifuatayo ni ombi lilipitishwa na Mkutano Mkuu mwaka wa 2010 unaohitaji wilaya za shule kujua ikiwa watoto wote katika familia wana bima ya afya au la.

Je, kila mtoto katika familia yako ana bima ya afya?

☐ NDIYO

☐ APANA

**MO HealthNet (Medicaid) inachukuliwa kama bima ya afya**.

Jibu likiwa ni Apana, wilaya ya shule itahitaji kujua ikiwa Mtoto Wako Anahitaji fomu ya Bima ya Afya kwa ajili ya familia.

Kwa kujua ikiwa unastahili kupewa chakula si shurti ujaze formu hii. Ombi la Chakula Bila Malipo na Bei Chini kwa familia itakaguliwa bila kujali jibu lako kwa taarifa ulizoombwa.

Baada ya kujaza fomu hii, irejeshe kwa shule/wilaya ya shule lako.

Jina la mzazi/mlezi: ______________________________

Anwani: ______________________________

Mji: ____________________ Jimbo: __________ Zip Code: __________

Idara ya Elimu ya shule za Msingi na Sekondari katika programu na shughuli zake haibagui kwa msingi wa jamii, rangi, dini, jinsia, asili ya kitaifa, umri au ulemavu. Maswali yanayohusiana na Programu za Idara na namna watu wenye ulemavu wanaweza kupata huduma, shughuli, na vifaa ni vizuri kuuuliza kwa Jengo la Ofisi ya Jimbo la Jefferson, Ofisi ya Mshauri Mkuu, Mratibu – Uzingatiaji wa Haki za Kiraia (Title VI/Title IX/504/ADA/age Act), Ghorofa la 6, 205 Jefferson Street, P.O. Box 480, Jefferson City, MO 65102-0480; namba ya simu 573-526-4757 au TTY 800-735-2966; barua pepe kwa civilrights@dese.mo.gov.

Saint Louis Public Schools 801 N. 11th Street St. Louis, MO 63101 314-345-4519